

Awamu ya BPS Kufunguliwa Kuanzia tarehe 1 Februari, 2021

Hoja Kuu

1. **Msimamizi na Bodi wanawataka wanafunzi wa BPS kurejea shuleni** punde tu itakapokuwa salama na kuwajibika kufanya hivyo. Tutachukua hatua kukufidia masomo yaliyopotea. Lakini hatuwezi kugeuza maisha na matokeo ya afya kwa umma, kwa kuweka wilaya nzima hatarini hivi karibuni.
 - Mpangilio wa msingi wa shule utaipa kipaumbele wanafunzi wenye mahitaji ya juu, Pre-K- 2, na wanafunzi waandamizi katika awamu 1 kwa kurudi kwetu kwa maelekezo.
2. Kulingana na Mkurugenzi wa Matibabu BPS Dkt. Dennis Kuo, Mkuu wa Kitengo cha Maendeleo ya Huduma za Watoto na Urekebishajii wa UBMD, **kusambaa kwa virusi kwenye jamii kwa sasa** kuko juu na hivi karibuni hali itakuwa mbaya zaidi. Dkt. Kuo anapendekeza kusomea mashinani hadi tarehe 1 Februari, kwa uthabiti wa masomo kwa muhula mmoja hadi wakati wa kufunguliwa kikakmilifu njia mpya za majaribio na pia kutia chanjo watoto 750 dhidi ya MMRV.
3. Kwa kuwa **BPS ilimakinika mnamo Machi** na kwa weledi ikageuzwa kwa mafunzo ya mbali pekee mara ya kwanza katika Jimbo la New York, kusambaa kwa haraka kwa hatua za kwanza za virusi kuliepukwa huko Buffalo. Tuko katika uamuzi sambamba kwa sasa.
4. BPS inachukua **hatua ya kushughulikia matukio na hisia ya kijamii** kutokana na kufungwa kulikosababishwa na Covid-19:
 - Wanafunzi wote wa BPS hushiriki katika **Social-Emotional Circle Time** kama njia ya kukamilisha kujiandikisha kijamii-mihemko na wanafunzi na kujenga ujuzi wa kukabiliana.
 - Kila shule ina **Wafanyakazi wa Jamii, Washauri na Wanasaikolojia** wanaowasaidia wanafunzi walio na wasiwasi kupitia huduma za ushauri nasaha kwa njia ya simu.
 - Kila shule imeunganishwa na **mshirika wa jamii ya afya ya akili** ili aatoe huduma za haraka za tiba ya simu ya afya ya akili ya mtu binafsi.
5. Masomo ya Mtandaoni **yanafanya kazi kwa ufanisi** wakati huu wa kufungwa:
 - Wilaya **imeidhinishwa na Kamishna wa Elimu** kama mbinu ya kujifunza mtandaoni na shule za BPS kadhaa na inagawanya mpangilio wetu jimbo zima.
 - Utulivu wa wafanyakazi ni wa kiwango cha juu kila wakati kumaanisha **kuwa wanafunzi wanapata wakati mwafaka wa masomo.**
6. **Matokeo ya msaada/elimu** mengine ya Robo 1 ni pamoja na:
 - **Gredi** za masomo ya msingi manne (hesabu, sayansi, masomo ya kijamii na ELA) 76% ya gredi zilikuwa za kupita; 18% ya gredi hazikuwa zimekamilika; 6% ya gredi hazikuwa za kupita.
 - **Viwango vya mahudhurio** vilikuwa mtawalia na shule 5 kubwa za wilaya; na sio mbali zaidi ya mtu anapokuwa kivyake. Kwa wastani 83% ya gredi ni za shule ya msingi na 78% ya gredi ni za wanafunzi wa shule ya upili
 - Ufuatiliaji wa wanafunzi wandamizi wa mwaka wa 2021 unaashiria kwamba tupo mbioni kuzidisha **kiwango cha kuhitimu** cha mwaka uliopita wa kiwango cha 76.2%
 - 97% ya wanafunzi **wanatumia kifaa cha BPS cha kusoma ukiwa mbali.** (Na hao 3% wengine wamechagua kutumia vifaa vyao wenyewe)
 - Wilaya imeimarisha ushirikiano wa **ubunifu wa ndani na serikali kusaidia muunganisho wa mtandao** kwa masomo ya nyumbani(kupitia vituo tarishi vya mtandao na huduma za broadband) bila malipo kwa kila nyumba na familia ya mwanafunzi